Kodi ya mimba, nani alipe?

Jishindie kompyuta ndani!

Kijitabu hiki kimetayarishwa na watendaji wa Tamasha kwa kushirikiana na Twaweza

Waandishi:
Richard Mabala na Winston Churchill Shauri

Mchoraji:
Daniel Mzena

Wahariri:
Rakesh Rajani, Evarist Kamwaga, Joseph Ngwegwe na Justice Rutenge

Usanifu:
Winston Churchill Shauri

©Tamasha/Twaweza 2012

Barua: S.L.P. 15044, Arusha, Tanzania
Simu: +255 719 751 928
+255 787 220 233

Barua pepe: rmabala@yahoo.com
wchachi@yahoo.com

Tovuti: www.tamashavijana.org

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni kunakili chanzo cha sehemu uliyonakilia na kutuma nakala mbili kwa Tamasha.

Utangulizi

Ndugu wasomaji,

Hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya aliwaagiza madiwani kutunga sheria ndogo za kuwakamata wanafunzi wa kike wanaopata mimba. Alisema:

"Wakilala ndani watawataja waliowapa mimba ndipo sheria za nchi zitafuatwa...Mpango wa kuwakamata waliowapa mimba wanafunzi hautoshi kukomesha tatizo hili, sasa tuwakamate na ninyi wenye mimba, labda tumwache aliyebakwa tu, lakini wengine mmepata kwa hiari yenu na hakuna sababu ya kutowachukulia hatua".

Kauli kama hizo zimetolewa na viongozi mbalimbali maana idadi ya wanaopata mimba inatisha. Kwa mujibu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika kipindi cha 2004-8, wasichana 28,590 wakiwepo 11,599 wa sekondari na 16,991 wa msingi walikatishwa masomo kwa sababu ya kupata mimba. Kutokana na ongezeko la shule za sekondari, yawezekana idadi inazidi kuongezeka.

Ni rahisi kuwalaumu wasichana wenyewe bila kuangalia mazingira yanayowasababishia kupata mimba. Katika utafiti wa kitaifa kuhusu ukatili dhidi ya watoto, iligundulika kwamba karibu theluthi ya wasichana wamenyanyaswa kijinsia. Kati yao, 5% wamelazimishwa kufanya ngono wakati ni watoto. Robo walisema kwamba walipofanya ngono mara ya kwanza, ama walidanganywa ama walishinikizwa ama walilazimishwa.

Hali hii inaonyesha kuna ulinzi dhaifu wa wasichana. Wao bado ni watoto, miili yao na akili zao hazijapevuka. Wengi sana wanadanganywa na wanaume wanaowazidi umri na mbinu.

Tufanye nini kukomesha hali hii?

Richard Mabala
Mkurugenzi, Tamasha

Wahusika

Bonge: Mjasiriamali, mchambuzi wa mambo na mkereketwa wa maendeleo

Bibiye: Mwelimishaji rika, mchambuzi na mwanaharakati

Mwenyekiti: Kiongozi anayesikiliza na kuheshimu vijana. Mpenda maendeleo lakini anaamini zaidi msaada kutoka nje kuliko nguvu ya wananchi

Mtendaji: Mchapakazi lakini mrasimu. Hapendi vijana na azma yao ya kuchukua hatua wenyewe

Rehema: Msichana aliyebakwa

Jamani baba unaniua...
... unaniua...
5
Kufa ibilisi wewe. Nilikupeleka shule usome siyo ufanye uhuni!

Kwenda huko kwa hayawani mwenzio. We si mtoto wangu tena.
Pole sana dada Rehema. Inuka twende kwangu.

Nilibakwa mie. Baba hataki kusikia.
Nani jamani?
Mwenye nyumba. Alipoona siwezi kulipa kodi, akanivamia.

Mwenye nyumba ni nani?
Si huyu mzee Matata. Amejenga nyumba tatu za kuwapangisha wanafunzi. Na tukishindwa kulipa...
Basi, basi, basi. Tulia.

Unajua huyu ni msichana wa kumi na moja mwaka huu. Mara waliimu, mara wenye nyumba, mara kutafuta pesa za matumizi. Aaaagh!
Haya wengine twendeni. Anahitaji mapumziko si umbea.

Kwa mshauri nasaha
Samahani jamani siwezi kufanya kitu. Ukitaka kushtaki ubakaji lazima uje mara baada ya tendo kutokea.
Najua mama. Lakini ameharibu maisha yake kabisa. Huyu si muanafunzi? Na ana miaka 16 tu.
Atatutambua! Watatutambua wote!

Lakini hakuna kushika jiwe wala kupiga yowe, mnasikia? kimya.

Wanazingira nyumba
Nimeita wanamgambo. Mtakoma ibilisi wakubwa nyie.

Ngoja. Kwani tunafanya fujo gani?
Huoni? Mnavuruga amani.
Mpaka kiongozi aje!

Vijana mnafanya nini?
Rehema anasema huyu mzee alimbaka na kumpa mimba. Lakini amekataa.
Usiwasikilize wahuni hao. Wanataka kuniharibia jina tu.
Ni wewe. unajua ni wewe.

Huyoooo!
Huyoooo!
Mkamate!

Sasa vijana tufanyeje? Hii ni nchi ya utawala wa sheria.
Tunataka iwe ya haki pia. Huyu mzee anavyonyemelea wanafunzi ni sheria au haki? Hata taarifa zake zingine nimazo.
Ni rahisi sana. Afungulive mashtaka.

Yaani jirani yetu amejenga karibu na shule ili atupate.
Shule mbali ndiyo maana inabidi tupange huko. Kisha wazazi hawana pesa za matumizi. Tufanyeje?
Na si huyu tu. Lakini hakuna anayetujali.

Kweli. Nyie viongozi mnajua hali hii. Au ni pesa zao...
Kijana hebu uwe na heshima! Hili suala lazima lijadiliwe katika kikao.
Sawa kabla ya kikao, tutakusanya habari zaidi.

Mwenyekiti, nimefurahi kwamba umeitisha mkutano huu. Bila kuwatia adabu hawa watoto wetu, watatharibika kabisa.
Ndiyo kutwa kurandaranda mitaani watasoma saa ngapi?
Mbona hivyo. Hebu tuwasikilize na wao.

Ya nini kuficha ukweli? Vijana wa siku hizi!
Ngoja. Tuliwaambia wasichana waandike kila wakitongozwa. Kwa wastani kila msichana ametongozwa mara kumi kwa siku.
Na wengi wamo humuhumu, walimu ...viongozi...wazee.

Na katika kukataa mara nyingi wanatishiwa kubakwa.
Huu ni uzushi mtupu. mnaji-tetea. Uhuni wenu tu!
Unataka nisome majina ya nani aliyetongoza, sag ngapi na wapi?

We kijana angalia vizuri unalosema. Walimu wangu hawawezi kufanya hivyo. Ni kinyume cha maadili ya walimu.
Nisome majina yao?
Mh! leo

Huu si mkutano wa kunyoosheana vidole. Binti zetu wana hali. ngumu. Na sisi wazazi tunaangalia badala ya kuchukua hatua.
Ndiyo. Hebu angalia ramani iliyochorwa na wasichana. Unaona X nyekundu? Ndiyo maeneo ya hatari.
Kila mahali ni hatari, isipokuwa kanisani na msikiti. Hata majumbani!

Kweli upangaji wa wasichana kwenye nyumba binafsi ni shida. Msichana akishi-ndwa kulipa kodi, aje kwetu mara moja.
Haitoshi. Watu washtakiwe. Enzi za kuachiwa zimekwisha.

Na waharibifu wajue. Kila anayejaribu atatukuta sisi. Lazima sisi vijana tuwalinde dada nzetu.
Vijana ndiyo Waharibifu Mnawavizia. wasichana wakiwa njiani kwenda shule au kuchota maji.
Tutawachukulia hatua na wao Tushirikiane badala ya kulaumiana.

Laiti tungekuwa na bweni kwa wasichana. Tuombe pesa wilayani kisha tujenge.
Ndiyo tusaidiane kujenga, lakini itachukua muda mrefu.
Sawa lakini tukomeshe tabia hii kwanza. Vinginevyo, hata bweni halitazuia.
Viongozi wa dini watusaidie katika hayo. Unyanyasaji ni dhambi kubwa sana.

Na ili kuhakikisha kwamba mambo hayo hayatokei shuleni, wanafunzi wata-mchagua mwalimu mmoja awe mlezi wao. Yeye ndiye atakayesikiliza masuala hayo.
Sawa, lakini haitoishi Hata kituo chetu cha vijana kitakuwa wazi kwa msichana yeyote mwenye matatizo.

Njoo hapa mwanangu. Laiti ningejua!
Hukutaka kujua mzee. Mlimfukuza. Lini tutajifunza kulea?

Kweli tuazimie pamoja ubakaji mwiko. ubakaji mwisho...
...Ubakaji... Ubakaji
Mwiiikoooo...
Mwiiishoooo...

Je wajua?

1. Unyanyasaji kijinsia wa mtoto unamwathiri kimwili, kimaadili, kihisia na kiakili kwa maisha yake yote. Anaweza kujiona duni, asijijali na kujipeleka kwenye vitendo hatarishi.
2. Kwa mujibu wa sheria, kufanya ngono na msichana chini ya miaka 18 inahesabiwa kuwa kosa la ubakaji. Hii ni kwa sababu bado hajakua vya kutosha kiakili na kimwili.
3. Licha ya sheria kali, ubakaji unazidi kushamiri, hasa kwa kuwa wabakaji huchukuliwa hatua mara chache.
4. Katika utafiti uliosimamiwa na Serikali
   a. Ubakaji hutokea zaidi saa za mchana.
   b. Majirani na wageni walitambulika kuwa wabakaji zaidi.
   c. Vijana wa kiume pia nao wanalazimishwa kufanya ngono.
   d. Nusu ya wasichana na theluthi mbili ya wavulana hawakumwambia mtu baada ya kunyanyaswa kijinsia.
   e. Asilimia 80 ya wasichana na asilimia 90 ya wavulana hawakutafuta huduma baada ya kunyanyaswa.
   f. Watoto walionyanyaswa kijinsia wako hatarini zaidi kuambukizwa UKIMWI kwa sababu ya kufanya ngono isiyo salama[1].
5. Katika utafiti wa TAMASHA:
   a. Wasichana walisema wanatongozwa angalau mara kumi kwa siku.
   b. Wasichana hawajaandaliwa kuhimili shinikizo kama hizo nyumbani wala shuleni.
   c. Wilaya ambapo wasichana wengi zaidi wanapanga chumba ili waende sekondari ndiyo wilaya ambapo kuna mimba nyingi zaidi.
6. Tukumbuke kwamba leo ni msichana yule, kesho ni mtoto wangu.

1 Takwimu zote zinatokana na Violence Against Children in Tanzania (URT, 2011)

Tufanye nini?

Kwanza, ni vizuri kufahamu hali halisi ya jamii yetu. Wasichana wanaweza kufanya utafiti kwa wasichana wenzao ili kupata picha kamili na pia wasichana wenyewe wanaona hatua gani zichukuliwe.

Katika jamii nyingine, viongozi wakishirikiana na vijana:

- Wanadhibiti ushiriki wa watoto katika maeneo hatari kama vile disko na video au ngoma za usiku wa manane.
- Wanafanya mipango ya kuwalinda wasichana hasa katika maeneo kama vile kwenda kisimani, kutafuta kuni au shambani.
- Wanawashirikisha vijana kuwalinda vijana wenzao.
- Wanachukua hatua dhidi ya wanaoonekana wananyasaji.

Shindano

Toa maoni, jishindie kompyuta!

Ndugu msomaji, hivi karibuni Serikali ya Tanzania imeahidi kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kupitia mpango huu, Serikali inataka kukusikia.

Toa maoni yako kuhusiana na upatikanaji wa huduma za msingi za kijamii; maji, elimu na afya.

Tuambie wazo moja kuboresha elimu, afya au maji. Halafu, tuambie mwananchi afanye nini kuleta mabadiliko.

Kila baada ya miezi mitatu kwa mwaka 2013, maoni kumi bora yatachaguliwa na kila shule itakayotoa washindi itapatiwa kompyuta ndogo mbili (laptops). Pia, maoni ya washindi yatachapishwa kwenye vitabu na tovuti.

Sharti: Kila mtu anaweza kutuma maoni, lakini zawadi zitatolewa kwa watakaondika *kupitia* shule zao tu.

Tuma maoni yako kabla ya tarehe 1 Novemba, 2013

Anuani: OGP Tanzania, S.L.P 38342, Dar es Salaam

Barua pepe: unasemaje@gmail.com

Kumbuka kuweka taarifa hizi:

- Tarehe
- Majina kamili, umri wako, jina la shule; jinsia (me/ke)
- Anuani kamili: SLP na makazi (kata, wilaya na mkoa); namba ya simu; barua pepe

Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi **(Open Government Partnership - OGP).**

Open Government Partnership

Mpango wa OGP unahimiza shughuli za Serikali ziendeshwe kwa uwazi zaidi ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, mwitikio wa Serikali, kupambana na rushwa na kujenga kuaminika zaidi. Twaweza inashirikiana na Serikali kuendeleza uwazi na ushiriki wa wananchi kupitia Mpango wa OGP.